AFRICAN UNION | **UNION AFRICAINE**

الاتحاد الأفريقي

UNIÃO AFRICANA

UMOJA WA AFRIKA | **UNIÓN AFRICANA**

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: 5517 700 Fax: 5517844
Website: www.au.int

BARAZA LA UTENDAJI
Kikao cha Kawaida cha Arobaini na Nne
Tarehe 15 Januari - 15 Februari 2024
Addis Ababa, ETHIOPIA

EX.CL/1461(XLIV)
Matini Chanzi: Kiingereza

TAARIFA YA SHUGHULI ZA MWAKA 2023 ZA KAMATI NDOGO YA PRC KUHUSU WAKIMBIZI, WAKIMBIZI WANAOREJEA NYUMBANI, NA WATU WALIOYAKIMBIA MAKAZI YAO

I. UTANGULIZI

1. Taarifa hii inawasilisha shughuli za Kamati Ndogo ya kamati ya Kudumu ya Wawakilishi (PRC) Kuhusu Wakimbizi, Wakimbizi Wanaorejea Nyumbani, na Watu Walioyakimbia Makazi yao (IDPs) kwa kipindi cha Januari 2023 hadi Desemba 2023. Shughuli hizi zilijikita kwenye mpango kazi ambao ulipitishwa na Kamati Ndogo katika mkutano wa wadau mnamo tarehe 13 Aprili 2023.

2. Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Wakimbizi, Wakimbizi Wanaorejea Nyumbani, na Watu Walioyakimbia Makazi yao ilitoa msaada, muongozo na uongozi katika shughuli zifuatazo: -

a. Kazi Maalumu za Ukadiriaji wa Mahitaji ya Kiutu kwa nchi Wanachama zilizochaguliwa ambazo ziliathiriwa na majanga ya Kiutu
b. Uendeshaji wa Shirika la Masuala ya Kiutu la Afrika (AfHA)
c. Ushiriki katika mikutano iliyoandaliwa na Idara ya Afya, Masuala ya Kiutu na Maendeleo ya Jamii (HHS)
d. Ushiriki katika Majukwaa ya Kimataifa yafuatayo:

II. KAZI MAALUM ZA UKADIRIAJI WA MAHITAJI YA KIUTU ZILIZOFANYWA MWAKA 2023

3. Mnamo mwaka 2023, Kamati Ndogo ya PRC Kuhusu Wakimbizi, Wakimbizi Wanaorejea Nyumbani, na Watu Walioyakimbia Makazi yao (IDPs) ilipanga na kufanya ziara za kikazi za uwandani kwa Nchi Wanachama saba wa Umoja wa Afrika na ilitoa ishara ya mshikamano kwa Nchi Wanachama nane yaani Burkina Faso (150,000), Eswatini (150,000), Ethiopia (150,000), Malawi (500,000), Mali (150,000), Msumbiji (150,000), Sahrawi (150,000), na Somalia (150,000). Tume iko katika mchakato wa kupeleka ishara hiyo ya mshikamano kwa Nchi ya Libya (500,000), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (150,000), Morocco (500,000), na Nigeria (150,000).

4. Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Mauritania hazikutembelewa kwa sababu Tume haikupata ruhusa kutoka kwa mamlaka za serikali kufanya kazi hizo maalumu katika nchi hizo.

5. Kazi maalumu nchini Libya, Ethiopia, Morocco, na Nigeria zitafanyika mwezi Novemba na Desemba 2023 ikiwa Tume itapata ruhusa kutoka kwa mamlaka husika.

TAARIFA MAALUM ZA NCHI

ESWATINI

6. Kazi Maalum ya Ukadiriaji wa Mahitaji ya Kiutu katika Ufalme wa Eswatini

ilifanywa kuanzia tarehe 26-29 Julai, ikiongozwa na Mhe. Alifre Ayele, Balozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia na Mwakilishi wa Kudumu katika Umoja wa Afrika. Balozi huyo alisindikizwa na Mkurugenzi wa Afya na Masuala ya Kiutu na Afisa kutoka Idara ya Masuala ya Kiutu.

7. Ujumbe ulionesha mshikamano wa Nchi Wanachama na Serikali na watu wa Eswatini na ulitoa dola za Marekani laki moja na elfu hamsini (Dola 150,000) kwa serikali na watu wa Eswatini na kuwahimiza kukabiliana na kutafuta suluhisho la kudumu kwa Watu Walioyakimbia Makazi yao.

8. Ujumbe wa AU ulikutana na Mhe. Chief Ndlaluhlaza, Kaimu Waziri Mkuu, Mhe. Mabulala Maseko, Kaimu Waziri wa Mambo ya Nje na ushirikiano wa Kimataifa, na Kaimu Waziri wa Mambo ya Ndani na Usimamizi wa Kitaifa wa Hatari ya Majanga.

Matokeo ya Ujumbe

9. Hali ya Kiutu katika Ufalme wa Eswatini ilisababishwa na Kimbunga Eloise ambacho kiliathiri maeneo manne (4) yaani, Hhohho, Manzini, Lubombo na Shiselwini. Hasara na uharibifu ulitokea kwenye miundombinu muhimu ambayo inajumuisha nyumba na mazao. Jambo hili lilizuia maisha ya wananchi na jamii zisizohamasishwa kwa sababu muunganiko kati ya jamii ulikuwa umeharibiwa.

10. Uharibifu kwenye miundombinu muhimu na ya msingi ulikuwa mkubwa na ulizuia utoaji wa huduma muhimu za kijamii kama vile afya, elimu, maji, nishati, usafiri na mawasiliano. Ujumbe ulitambua kuwa nchi ilikumbwa na vifo 4, watu walioathirika 2,768, nyumba 777, madaraja 53 na km 774 za miundombinu ya barabara zilikuwa zimeharibiwa. Makadirio ya hasara ya kifedha yalikisiwa kuwa takriban Emalangeni ya Eswatini milioni 500.

Changamoto

11. Nchi ililazimika kuelekeza rasilimali zilizokusudiwa kwa ajili ya maendeleo kwenye kushughulikia rasilimali na kupunguza athari za Kimbunga Eloise. Jambo hili litaathiri kwa kiasi kikubwa mipango ya maendeleo ya nchi. Kwa kuongezea, ukosefu wa rasilimali za kutosha ulipunguza uwezo wa nchi wa kuitikia kwa haraka kwenye majanga ya Kiutu. Pia, kutokana na kuendelea kuwepo kwa hali mbaya ya hewa, jitihada za ujenzi upya zilizorota jambo ambalo lilizidisha vikwazo kwenye maunganisho na marekebisho kwenye miundombinu muhimu.

Mapendekezo

12. Ujumbe ulipendekeza kuwa Umoja wa Afrika na wabia wanapaswa kuisaidia Serikali ya Eswatini na Shirika la Taifa la Usimamizi wa Majanga katika kujenga uwezo kuhusu Usimamizi wa Hatari ya Majanga na Ustahimivu, na katika uratibu wa baina ya sekta kwa ajili ya tahadhari ya mapema na hatua ya mapema.

MALAWI

13. Kimbunga cha kitropiki cha Freddy kiliharibu Jamhuri ya Malawi kwa vile kilisababisha vifo visivyopungua 676 na kuathiri zaidi ya watu milioni mbili (2) na kusababisha uharibifu kwenye barabara na miundombinu muhimu.

14. Kufuatia mwaliko kutoka Serikali ya Malawi, Kamati Ndogo ya PRC Kuhusu Wakimbizi, Wakimbizi Wanaorejea Nyumbani, na Watu Walioyakimbia Makazi yao (IDPs) ilifanya ziara ya uwandani ya Kiutu nchini Malawi kuanzia tarehe 23-27 Aprili 2022. Ujumbe huo uliongozwa kwa pamoja na Mhe. Minata Samate Cessouma, Kamishna wa Afya, Masuala ya Kiutu na Maendeleo ya Jamii na Mhe. Mahlaba Ali Mamba, Balozi wa Ufalme wa Eswatini na Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Wakimbizi huku wakisindikizwa na maafisa kutoka Kurugenzi ya Afya na masuala ya Kiutu.

15. Ujumbe wa AU nchini Malawi ulikutana na Mhe. Lazarus Chikwera, Rais wa Jamhuri ya Malawi, na pia ulikutana na Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Malawi. Ujumbe wa AU uliwasilisha hundi ya dola za Marekani laki tano ($500,000.00) kama ishara ya mshikamano kutoka kwa Nchi Wanachama katika kushikamana na kusaidiana kwa ajili ya majanga yaliyowakumba.

16. Ujumbe wa AU ulifanya ziara za uwandani katika milima ya Chilombe na Soche ambayo ni maeneo yaliyoathiriwa zaidi na kutembelea kambi za watu Walioyakimbia makazi katika maeneo hayo. Ujumbe ulikutana na watu Walioyakimbia makazi kwenye kambi na kuonesha sikitiko lao kwa janga hilo. Ujumbe pia ulikutana na UN na wabia, ambapo Kamishna alitoa shukrani kwa msaada wao wa kuweza kuwa na mwitikio wa haraka na wa muda mfupi kwenye uharibifu mkubwa wa Kimbunga Freddy.

17. Ujumbe wa AU ulifanya mkutano na waandishi wa habari, ambapo kamishna aliipongeza serikali ya Malawi kwa mwitikio wao na kazi inayoendelea katika kupunguza, kubadilisha, kuhamisha na maisha stahimivu yanayoendelea kwenye jamii zilizoathirika. Pia Kamishna alirejelea ishara ya mshikamano ya Tume na kuwaomba wabia kuendelea kuisaidia nchi hiyo.

Matokeo ya Ujumbe

18. Ujumbe ulitambua kuwa kumekuwepo vifo 681 vilivyothibitishwa, watu waliopotea 578, majeruhi zaidi ya 2000, na watu zaidi ya 600,000 Walioyakimbia makazi. Kijiji kimoja kilisombwa kabisa, na miundombinu iliharibiwa vibaya sana.

19. Serikali ilitumia jeshi kusaidia kupitia jitihada za kuokoa maisha, jitihada za uokoaji, na ukarabati wa haraka wa miundombinu. Uwekaji makazi unaendelea, huku jamii zilizoathirika vibaya zikihifadhiwa kwenye kambi mbalimbali. Moja kati ya mahitaji muhimu sana ni hifadhi. Ili kushughulikia hitaji hilo la haraka, serikali na wabia wake

walifanya zoezi la kukadiria mahitaji na kuandaa mpango wa mwitikio wa miezi mitatu. Mpango huu wa mwitikio umepitishwa na kwa sasa uko unatekelezwa. Nchi Wanachama katika ukanda wa SADC, Serikali, Wabia, na Asasi za Kiraia zimekuwa zikichangia kutoa msaada kwa familia zilizoathirika kwa kutoa hifadhi, chakula, elimu, afya, na msaada wa kisaikolojia na kijamii.

Changamoto

20. Malawi inakabiliwa na athari za Kiutu za majanga ya asili yanayopelekea kwenye ulazima wa kujenga upya nyumba, barabara, shule, vituo vya afya, utawala wa umma, na huduma za umma. Kiwango hicho cha ujenzi upya kinahitaji uwezo mkubwa wa kifedha ili kujenga upya vizuri miundombinu yote katika maeneo yaliyoathiriwa.

Mapendekezo

a. Msaada zaidi unapaswa kutolewa ili kuwezesha jitihada za serikali katika kushughulikia changamoto za Kiutu zinazosababishwa na majanga ya asili. Zaidi ya hayo, msaada wa kimaendeleo unahitajika ili kurahisisha kurudi, kutangamana tena, na ukarabati pale inapowezekana.

b. Nchi inahitaji kuboresha mfumo wake wa uratibu ili kuifanya kuwa fanisi zaidi katika kushughulikia changamoto ambazo inaweza kukutana nazo.

c. Nchi inaweka mkazo kwenye kuwawekea makazi mapya IDPs kwenye maeneo salama na yenye hatari kidogo. Hata hivyo, ili kupata suluhisho la kudumu, jambo hili linapaswa kufanywa kwa kushauriana, kujadiliana na kushirikiana na IDPs. Watu ambao walikimbia makazi yao kwa nguvu huwa wanarudi kwenye ardhi yao ya asili, licha ya kuwepo hatari kubwa. IDPs wanapaswa kupewa taarifa, kuelimishwa, na kushauriana nao kabla ya kupewa makazi mapya.

d. Wito kwa Jumuiya ya Kimataifa hususan wabia wa Kiutu na maendeleo, yakiwemo mashirika ya UN na mashirika ya kimataifa, kuendelea kuisaidia serikali katika jitihada zake za kujenga upya miundombinu iliyoathiriwa na katika kutafuta suluhisho la kudumu la athari za majanga.

MALI

21. Kamati Ndogo ya PRC Kuhusu Wakimbizi, Wakimbizi Wanaorejea Nyumbani, na Watu Walioyakimbia Makazi Yao (IDPs) ilifanya kazi maalum ya ukadiriaji nchini Mali ikiongozwa na Mhe.Jainaba Jagne, Balozi wa Jamhuri ya Gambia nchini Ethiopia na Mwakilishi wa Kudumu katika Umoja wa Afrika na Tume ya Uchumi kwa ajili ya Afrika kuanzia tarehe 5-9 Februari 2023. Balozi huyo alisindikizwa na afisa kutoka Idara ya Masuala ya Kiutu.

22. Ujumbe huo nchini Mali ulifanya mikutano na wadau wapiga mbizi akiwemo

Rais wa Serikali ya Mpito, Waziri Mkuu wa Serikali ya Mpito, Mh. Choguel Kokalla Maiga; Waziri wa Mambo ya Nje Ndugu Abdulaye Diop, mwakilishi wa Waziri wa Afya na Maendeleo ya Jamii, anayeshughulika na misaada ya Kiutu, mshikamano, wakimbizi na watu Walioyakimbia makazi yao Ndugu Oumarou Diarra pamoja na mashirika ya Umoja wa Mataifa na watu waliathiriwa.

23. Ujumbe huo pia ulifanya ziara kwenye kambi za wakimbizi/watu Walioyakimbia makazi yao hususan kambi za Meneka na Gao. Ziara hizi zililenga kuimarisha uratibu wa mwitikio wa Kiutu katika maeneo hayo mawili; kuwahimiza wadau muhimu wa kiraia au wa kijeshi, ili kuwezesha zaidi ufikiaji wa watu wenye mahitaji. Kwenye kambi za Gao na Menaka, ujumbe huo ulifanya mazungumzo na mamlaka za maeneo hayo na washauri wa muda wa maeneo hayo, lakini pia na watendaji wa Kiutu. Ujumbe huo ulitembelea miradi na makazi ya watu Walioyakimbia makazi yao, na kufanya nao mazungumzo kuhusu hali zao za maisha na mahitaji ambayo bado hawajatimizwa.

Matokeo ya Ujumbe

24. Katika kipindi kilichoangaziwa na taarifa hii mwezi Februari 2023, hali ya Kiutu nchini Mali inakabiliwa na mzozo tata ulioathiri nchi hiyo na kuchagizwa na mgogoro, ukosefu wa usalama, na matukio ya tabianchi, ambayo yamesababisha idadi kubwa ya watu kuhama makazi yao, kudorora kwa uthabiti wa kijamii na kisiasa, matukio ya tabianchi na magonjwa ya milipuko na viwango duni vya usalama wa chakula na lishe ambavyo havijawahi kutokea. Katika kipindi cha ujumbe huo, tishio la usalama lilitokana na migogoro ya kikabila, mashambulizi ya silaha kutoka kwa vikundi visivyo ya serikali dhidi ya raia, mashambulizi ya makundi yenye itikadi kali na baina ya makundi ya waasi na makundi ya kijamii. Mali pia inakabiliwa na ukame ambao umeathiri zaidi usalama wa chakula. Nchi hiyo ina matukio ya ukiukaji wa haki za binadamu na ukiukaji wa Sheria za Kiutu za Kimataifa. Mashambulizi ya kikatili yanayofanywa na waasi yameathiri raia, ambapo watu wapatao milioni 8.8 wameathiriwa na wanahitaji misaada ya Kiutu, sawa na asilimia 42% ya raia wa Mali.

25. Katika maeneo ya Gao na Ménaka, mapigano yanayoendelea miongoni mwa makundi yenye itikadi kali karibu na makazi ya raia ni changamoto ya kiulinzi, pamoja na ongezeko la tishio kutoka kwa makundi hayo kwa jamii kuimarisha ushawishi wao. Dola la Kiislamu kwenye eneo kubwa la Sahara ni kichochezi kikuu cha ukatili, ambapo mashambulizi na tishio katika maeneo mengi ya jamii za Djebok na Gabero katika wilaya ya Gao, Talataye na Tin Hama huko Ansongo *cercle* mkoa wa Gao, na Anderamboukane, Emis Emis na Inékar katika mkoa wa Ménaka.

26. Kuongezeka kwa changamoto ya ulinzi kuna athari hasi kwa hali ya Kiutu ambayo tayari ni mbaya. Idadi ya watu Walioyakimbia makazi yao iliongezeka kutoka 350,000 hadi 397,000 katika maeneo ya katikati na kaskazini mwa nchi, ilhali zaidi ya wakimbizi 175,000 wa Mali walikuwa katika nchi za jirani. Zaidi ya watu milioni 1.8 wana hali mbaya

ya usalama wa chakula na watoto milioni 2 wenye umri chini ya miaka mitano wameathiriwa na utapiamlo. Wakati watendaji wa Kiutu wakifanya jitihada kubwa kutoa huduma za chakula, malazi na afya kwa watu waliobainika kuhama makazi yao, upatikanaji wa raslimali unaendelea kuwa changamoto kubwa.

27. Ujumbe ulibaini kwamba jitihada za serikali ya mpito kutoa ulinzi, misaada na malazi kwa watu Walioyakimbia makazi yao ni mdogo kwa sababu ya ukosefu wa fedha; hata hivyo, Kurugenzi ya Taifa ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Wadau wengine inajitahidi kuboresha hali ya maisha ya watu waliohifadhiwa kwenye kambi.

28. Serikali imeonesha utekelezaji kwa vitendo wa Mkataba wa Kampala wa mwaka 2009, na Mkataba wa OAU wa mwaka 1969 ambao unadhihirisha uhamilishaji wa mwongozo wa Umoja wa Afrika lakini unahitaji msaada kutoka kwa mashirika ya Umoja wa Mataifa yanayofanya kazi katika maeneo hayo ili kuboresha hali za watu Walioyakimbia makazi yao na kuwapa mahitaji yao.

29. Wakati wa ziara hiyo, ujumbe huo ulibaini kwamba hakuna mikakati inayolenga kuwawezesha wakimbizi na watu Walioyakimbia makazi kujitosheleza wenyewe kwa njia ya kipato, kilimo na shughuli zingine za kujikimu, hasa kutokana na ufikiaji hafifu wa huduma za chakula, afya na elimu.

Changamoto

30. Changamoto kubwa nchini Mali ni pamoja na mizozo inayoingiliana na kuchagizwa na mitikisiko ya kisiasa, tabianchi, magonjwa na usalama ambayo imekatiza usambazaji wa huduma muhimu za kijamii kwa raia na kuhujumu juhudi za maendeleo.

Mapendekezo

a. Himiza pande zinazohusika kufanya mazungumzo ya kisiasa ili kutatua migogoro inayoendelea nchini humo, tekeleza mpito wa kisiasa kwa amani, na kujenga mazingira mazuri kwa watu kurejea kwenye makazi yao, kurejesha hali zao za awali na kuwajumuisha watu walisio na makazi na wakimbizi katika hali ya usalama na yenye kuzingtia utu.

b. Saidia serikali ya Mali kubuni na kutekeleza miradi ambayo inalenga mahitaji muhimu ya walkimbizi na watu wasio na makazi kwa kuongeza ushiriki wa wadau. Ili kufikia lengo hili, washirika wa Kiutu na wadau muhimu wanapaswa kulenga na kuboresha usalama, upatikanaji wa vifaa vya shule na elimu, vituo vya afya na huduma za afya, maji na usafi wa mazingira.

MSUMBIJI

31. Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Wakimbizi, Wakimbizi Wanaorejea na Watu Walioyakimbia Makazi ilifanya ziara ya Tathmini ya Kiutu nchini Msumbiji kuanzia tarehe 05 hadi 11 mwezi Agosti 2023 kutathmini hali ya jumla ya Kiutu nchini humo kwa kuzingatia hali katika jimbo la kaskazini la Cabo Delgado. Ujumbe huo uliongozwa na Mh. Lamine Yahiaoui, Balozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kiarabu ya Saharawi, ambaye pia ni Mjumbe wa wakala wa Kamati Ndogo ya PRC kuhusu wakimbizi, Wakimbizi Wanaorejea nyumbani na watu wasio na makazi.

32. Ujumbe huo ulibadilishana mawazo na wadau mbali mbali akiwemo mwakilishi wa Wakala wa Taifa wa Usimamizi wa Dharura, maofisa kutoka wizara ya mambo ya nje, OCHA na mamlaka za ndani kutoka makao makuu ya jimbo la jimbo la Cabo Delgado huko Pemba.

33. Ujumbe pia ulifanya ziara kwenye kambi za watu wasio na makazi zilizopo kwenye jimbo la Cabo Delgado kutathmini hali za watu wasio na makazi.

Matokeo ya Ujumbe

34. *Tangu mwaka 2017, Cabo Delgado, jimbo la kaskazini zaidi mwa Msumbiji, ni kiini cha uasi wenye madhila makubwa*. Waasi wa Kiislamu, wanaojulikana kama al-Shabab (japo hautofautiani na kundi linalojukana hivyo nchini Somalia), limeingia mwaka wake wa saba. Tangua walipoanza mashambulizi yao mwezi Oktoba 2017, wanamgambo kwenye jimbo la kaskazini la Cabo Delgado nchini humo lenye utajiri wa raslimali wameua watu zaidi ya 4,500 na wengine zaidi ya milioni moja kuhama makazi hayo, wengi wao wakiwa wanawake na watoto. Majeshi ya Rwanda nan chi nyingine za ukanda wa kusini mwa Afrika yamesaidia kukubiliana na uhasi huo. Hata hivyo, ukatili wa kundi hilo dhidi ya raia umeendelea, na mwezi Mei 2022, Kamandi kuu ya Dola la Kiislamu (ISIS) lilitambua al-Shabab kama moja ya majimbo yake. Pamoja na kwamba wamedhoofishwa kiasi cha kuacha mashambulizi yenye hatari, kama ambavyo imekuwa miaka iliyopita, waasi hao wanaendelea kutumia mbinu za waasi na kuwa tishio siyo tu kwa Msumbiji pekee bali pia kwa nchi nyingine katika ukanda huo.

35. Jimbo la Cabo Delgado limekuwa na migogoro kwa muda mrefu. Vyanzo vikuu vya mgogoro ni pamoja na kutengwa kijamii na kiuchumi na kukataliwa kwa ushawishi wa wanajeshi walioshiriki katika vita vya ukombozi ambao wana maslahi ya kibiashara katika jimbo hilo. Jimbo la Cabo Delgado ni miongoni mwa majimbo ya Msumbiji yaliyo maskini zaidi, ingawa kuna raslimali nyingi za madini na gesi, ambazo zinadhaniwa kuwanufaisha zaidi watawala. Wengi wa wanachama wa al-Shabab walivutiwa kujiunga na uasi kwa nia ya kunufaika kiuchumi kwa kunyakua madaraka. Kundi hilo lilikua kwa kasi na kuwa na nguvu, na hivyo kuwa tishio kwa udhabiti wa kitaifa na kikanda.

36. Wakati wa ziara ya Pemba na miji ya karibu, ujumbe ulibaini kwamba umaskini na kutengwa kijamii na kiuchumi ni baadhi ya sababu za mgogoro ambazo zinahitaji

kushughulikiwa. Inakisiwa kwamba watu 945,000 wamehama makazi yao kutokana na makabiliano ya silaha katika jimbo la Cabo Delgado Province kaskani mwa Msumbiji, jambo ambalo linaendelea kuongeza mahitaji ya Kiutu.

37. Katika majimbo matatu ya kaskazni ya Cabo Delgado, Nampula na Niassa, mgogoro huo umeacha watu zaidi ya milioni moja bila chakula cha kutosha, wakiwemo watu wasio na makazi na familia zinazowahifadhi. Idadi kubwa ya vituo vya afya vimeharibiwa au kuteketezwa, na hivyo kuathiri uwezo wa kubaini na kuitikia mlipuko wa magonjwa, na kutoa huduma kwa wakati.

Changamoto

38. Ukiachilia mbali watu kuhama makazi yao kaskazini mwa Msumbiji, nchi hiyo ina historia ya vimbunga vya mara kwa mara, mafuriko na ukame. Kipindi cha msimu wa mvua mwaka 2022, nchi hiyo ilipigwa na matukio manne ya hali mbaya ya hewa, na hivyo kuathiri zaidi ya watu milioni moja na kuharibu miundombinu binafsi nay a umma. Ukame, ambao unajitokeza mara nyingi zaidi, ni changamoto kubwa kwa Msumbiji, kwa kuwa asilimia 80 ya raia wote nchini humo wapato milioni 32 hutegemea kilimo kinachotegemea mvua.

Mapendekezo

a. Msaada zaidi hauna budi kutolewa ili kuimarisha jitihada za serikali katika kushughulikia changamoto za Kiutu zinazosababishwa na uasi katika jimbo la Cabo Delgado.

b. Umoja wa Afrika na washirika waendelee kusaidia nchi hiyo kutekeleza Mkataba wa Kampala katika maeneo yaliyoathiriwa na watu kuhama makazi yao.

c. Wito unatolewa kwa Jamii ya Kimataifa hasa washirika wa Kiutu na maendeleo, ikiwemo wakala na mashirika ya Umoja wa Mataifa, kuendelea kusaidia serikali katika jitihada zake za kusaidia watu wasio na makazi kwenye maeneo yaliyoathirika.

WAKIMBIZI WA SAHRAWI NCHINI ALGERIA

39. Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Wakimbizi, Wakimbizi Wanaorejea Nyumbani, na Watu Walioyakimbia Makazi yao ilifanya Tathmini ya Mahitaji ya Kiutu kuanzia tarehe 7 hadi 12 Agosti 2023 kwenye kambi za wakimbizi nchini Algeria. Ujumbe huo uliongozwa na Mh. Mahlaba Ali Mamba, Balozi wa Falme ya Eswatini nchini Ethiopia, na Mwakilishi wa Kudumu kwenye Umoja wa Afrika na Kamisheni ya Kiuchumi kwa Afrika. Kiongozi huyo alifuatana na maofisa kutoka Kurugenzi ya Afya na Masuala ya Kiutu.

40. Ujumbe huo ulimtembelea Mh. Burchrya Beyond, Waziri Mkuu, Mh. Mohamwd Moulud, Waziri wa Fedha, Mh. Mohamed Yahia, Mkurugenzi Mkuu wa Chama cha Mwezi Mwekundu cha Sahrawi, Mh. Adda Ahmeim, Gavana wa Smare, na Mh. Jura Bulahi, Gavana wa Aswerd. Walitembelea pia Chama cha Taifa cha Watu Waliowekwa Kizuizini na Wafungwa, Wizara ya Usafirishaji, Wizara ya Raslimali Maji, na kambi za wakimbizi za Smare na Aswerd.

Matokeo ya Ujumbe

41. Hali ya kiutu kwenye kambi ya wakimbizi ya Tinduf imedumu kwa takriban miaka 25 na kama ilivyo kwa migogoro mingine ya muda mrefu barani Afrika, hali hii inakumbwa na upungufu wa msaada wa kifedha kwa ajili ya mipango ya kambi hiyo. Watu wanaoishi katika kambi hizi wanajishughulisha na shughuli za kujipatia kipato, kilimo, na uzalishaji wa kazi za sanaa kujaliza pengo la kifedha na kukidhi mahitaji.

42. Chama cha Mwezi Mwekundu cha Sahrawi kina msambao mzuri wa mtandao ambao unachangia asilimia 85% ya uendelevu wa wakimbizi katika kambi mbalimbali. Elimu, usalama na miundombinu muhimu ya ulinzi na msaada kwa watu wasio na makazi vinatolewa na nchi inayotoa hifadhi.

Changamoto

43. Hali hii inakolezwa zaidi na kukosa makazi kwa muda mrefu na hivyo kuathiri utoaji fedha kwa ajili ya huduma za kiutu. Nchi inayotoa hifadhi inalazimika kujenga uwezo wa wakimbizi wa kuzalisha kipato kwa ajili ya kujikimu.

Mapendekezo

a. Nchi inayotoa hifadhi na wadau wa Kiutu hawana budi kutoa na kutanua fursa za kiuchumi zenye kufaa zaidi kulingana na mazingira yaliyopo kwa ajili ya wakimbizi na maeneo yanayozunguka kambi kutokana na hali ya ukame ili kuboresha hazi za maisha ya wakimbizi.

b. Mimea na mifumo yenye kutunza maji inahitajika ili kuvuna na kutumia tena maji kidogo yaliyopo wakati wa hali ya ukame. Kazi hii haina budi kufanywa kwa kiwango kikubwa.

c. Programu za kuendeleza na kuwaajiri vijana hazina budi kutolewa shuleni, hususan katika ujuzi na maarifa ya kidijitali.

d. Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliyomo Afrika hayana budi kuhimizwa kuimarisha ubia na ushirikiano na Chama cha Mwezi Mwekundu cha Sahrawi na kuongeza uwepo wao kwenye kambi za wakimbizi.

e. Uwezeshaji na usaidizi wenye kuzingatia mahitaji unahitajika kwa Chama cha Mwezi Mwekundu cha Sahrawi, ikiwemo kubadilishana uzoefu na kutumia wataalam.

SOMALIA

44. Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Wakimbizi ilifanya tahmini ya Kiutu katika Jamhuri ya Somalia kuanzia tarehe 9 hadi 15 Septemba 2023. Ujumbe huo uliongozwa na Mh. Jainaba Jagne, Balozi wa Gambia nchini Ethiopia na Mwakilishi wa Kudumu kwenye Umoja wa Afrika na Kamisheni ya Uchumi kwa Afrika. Kiongozi huyo alisaidiwa na maofisa kutoka Idara ya HHS na wengine kutoka Mpango wa Mpito wa AU nchini Somalia (ATMIS).

45. Ujumbe huo ulikutana na maofisa kadhaa wa serikali, akiwemo Mh. Ahmed Yusuf Ahmed, Waziri wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi, Mh. Hamza Abdi Barra, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Somalia na Mh. Safia Hassan Mohamed, Kamishna wa Kamisheni ya Taifa ya Wakimbizi, Watu Wasio na Wakazi na Wanaorejea Nyumbani, na mtendaji wa Mashirika ya Kiraia. Ujumbe huo pia ulikutana na mashirika ya Umoja wa Mataifa na washirika wa Kiutu wanofanya kazi nchini humo ambao walitoa maelezo mafupi kuhusu ukubwa wa athari za ukame na njaa nchini humo ambazo zinawakumba watu takriban milioni 7.8, sawa na takriban nusu ya watu nchini humo. Somalia ina changamoto kubwa ya Kiutu na inazidi kuongezeka kutokana na matukio ya tabianchi ambayo yanaiathiri nchi hiyo. Ujumbe huo pia ulikutana na wawakilishi wa balozi za Nchi Zinazochangia Wanajeshi (TCC).

Matokeo ya Ujumbe

46. Somalia inakabiliwa na hali tete ya Kiutu, ambapo watu milioni 5 wanahitaji msaada wa Kiutu, ikiwemo zaidi ya watu milioni 2 walioathiriwa na na watu 320,000 Walioyakimbia makazi yao kutokana na ukame uliokithiri. Mvua zimekwama kwa kiasi kikibwa katika maeneo mengi ya Somalia, na kusababisha mavuno duni kuwahi kushuhudiwa. Vifo vya mifugo na bei kubwa za nafaka pia zimeshuhudiwa.

47. Hali ya ukame katika maeneo ya kusini mwa nchi hiyo ilidorora kwa kiasi kikubwa, ilhali katika maeneo mengine hali ilikuwa mbaya hadi ya wastani. Visima vya maji vinakauka kadri ujazo wa mto Juba na Shabelle unavyozidi kupungua kwa viwango vya juu. Bei za maji zimepanda kwa kiwango cha juu, ambapo sehemu za mashariki na kati za Majimbo ya Galmudug, Jubbaland, na Majimbo ya Kusini Magharibi yameshuhudia bei za juu zaidi za nafaka.

48. Ukame umedhoofisha shughuli za kiuchumi, hususan kwa sababu watu walio katika mazingira hatarishi zaidi wameshuhudia uwezo wao wa kurejea katika hali ya kawaida ukipungua kutokana na madhila ya muda mrefu ya migogoro, mitikisiko ya

tabianchi, na milipuko ya magonjwa. Asilimia 75 ya Wasomali wanaendelea kuishi chini ya mstari wa umaskini. Ukame wa sasa na ukosefu mkubwa wa maji na kukosekana kwa miundombinu ya usafi wa mazingira vimeongeza hatari ya kutokea magonjwa ya milipuko, ikiwemo kuhara na kipindupindu, hasa katika kambi za watu wasio na makazi na maeneo yaliyoathirwa na migogoro.

49. Ukosefu mkubwa wa chakula umeendelea kusababisha vifo vya Wasomali katika hali ya ukame wa vipindi vingi ambao haujashuhudiwa mashariki ya pembe ya Afrika. Endapo mashirika ya serikali na wafadhili wa kimataifa watashindwa kutoa misaada ya hali ya juu ya kifedha katika siku za usoni, vifo vinavyotokana na njaa vinaweza kuzidi vile vilivyotokana na njaa iliyopita nchini Somalia – ambapo watu takriban 260, 000 walikufa.

Changamoto

a) Changamoto kubwa ni pendekezo la kupunguza idadi ya wanajeshi wanaolinda amani nchini humo kwa kuwa inahofiwa kwamba hali hii inaweza kusababisha ukosefu wa usalama kwa kiasi kikubwa kwa watu walio katika hatari (wakimbizi na watu Walioyakimbia makazi yao).

b) Nchi hiyo imeathriwa na usalama mdogo wa chakula unaotokana na ukame na njaa kwa sabubu ya mvua zisizotabirika, mvua kidogo au kukosekana kabisa kwa mvua.

c) Somalia inakumbwa na ukosefu wa fedha, hasa kwa ajili ya watu wasio na makazi, na hivyo, hatua zinachukuliwa na washirika pale tu ambapo kuna wawakilishi wa ATMIS na UNSOS. Vilevile kuna pengo katika ufadhili wa kifedha na hivyo kuathiri mwitikio kamilifu kwa idadi kubwa ya watu wanaohama makazi kutokana na majanga yanayosababishwa na migogoro na tabianchi.

Mapendekezo

d) Umoja wa Afrika na jamii nzima ya kimataifa haina budi kuhamasisha misaada ya haraka ya Kiutu kwa Somalia na kuwezesha na kuhimiza suluhu ya kudumu ya watu kuhama makazi yao nchini Somalia.

e) Kuna haja ya kuhimiza serikali kujumuisha mahitaji ya Kiutu kwenye mipango ya kitaifa.

III. USHIRIKI KATIKA SHUGHULI NYINGINE NDANI YA MAJUKUMU YA KAMATI NDOGO YA PRC KUHUSU WAKIMBIZI

50. Mbali na tathmini ya hali ya Kiutu, Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Wakimbizi, Wakimbizi Wanaorejea Nyumbani, na Watu Walioyakimbia Makazi pia ilishiriki katika shughuli nyingine zilizo ndani ya majukumu yao kama ifuatavyo: -

a) Kamati hii ilishiriki kwenye Jukwaa la Mwaka la Vijana lililofanywa kwa pamoja na office ya Balozi wa Vijana wa AU, ambalo lilifanyika tarehe **15 hadi 17 Mei 2023** nchini Madagascar, ambapo vijana walitumia muda, maarifa na utaalam wao kwa kujitolea katika changamoto za kiutu barani Afrika, kuhamasisha haja ya watu walioathiriwa na migogoro ya Kiutu barani Afrika; matumizi ya teknolojia na ubunifu katika mwitikio wa kiutu na kuwa mfano kwa uongozi katika mwitikio wa kiutu barani Afrika.

b) Siku ya Wakimbizi Afrika/Duniani – tarehe **20 Juni 2023** iliadhimishwa chini ya kaulimbiu “Tumaini mbali na Nyumbani: Dunia ambapo wakimbizi wanajumuishwa mara zote” na kusisitiza masuala maalum ya kuwajumuisha wakimbizi barani Afrika. Idara kwa kushirikiana na shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia wakimbizi (UNHCR) liliunda jopo kwa ajili ya kuzungumzia suala hili.

c) Wajumbe wa Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Wakimbizi pia ilishiriki kwenye programu ya kujenga uwezo kuhusu mfumo wa kiutu Afrika: Sheria na Sera iliyofanyika kuanzia tarehe **28 hadi 30 Agosti 2023** mjini Bujumbura Burundi.

d) Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Wakimbizi ilishiriki mkutano wa wataalam ambao walifanya kazi ya kujumuisha mawazo ya Nchi Wanachama kwenye rasimu ya Mkataba kuhusu Kukosa Uraia ambao ulifanyika tarehe **4 hadi 5 Septemba 2023** mjini Cape Town Africa ya Kusini.

e) Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Wakimbizi pia ilihudhuria Wasilisho la Pembeni mjini New York, Marekani tarehe **21-22 Septemba 2023**, kuhusu “gharama ya kutochukua hatua nchini Sudani” ambapo mapendekezo kadhaa yalitolewa kuhusu hali nchini Sudani. Wasilisho lingine lililofanywa na Ujumbe wa Uswisi kwenye Umoja wa Mataifa lilijadili ulinzi wa raia barani Afrika na kupendekeza njia za kutatua changamoto zinazoambatana nalo.

f) Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mh. Mahlaba Ali Mamba, alihudhuria Kikao cha 74 cha Kamati ya Utendaji ya Programu ya Mabalozi tarehe **4 - 9 Oktoba 2023** mjini Geneva, Uswisi, ambapo nchi zote zilihudhuria na kutoa taarifa kuhusu hali ya kiutu yao. Nchi nyingi za Afrika zilitoa taarifa kuhusu jitihada zinazofanyika kutoa hifadhi kwa wakimbizi katika nchi zao huku kukiwa na upungufu wa ufadhili wa kifedha wa kimataifa.

g) Wajumbe wa wakala wa Kamti Ndogo ya PRC kuhusu Wakimbizi na wale waliofanya tathmini ya kiutu katika kipindi cha mwaka mzima wakishiriki kwenye Kongamano 11 la Mwaka la Kiutu lililofanyika mwishoni mwa mwezi **Novemba 2023** mjini Nairobi, Kenya, na kuwaleta pamoja Wadau waote wa Kiutu kushughulikia hali ya kiutu barani Afrika.

h) Mwezi **Disemba 2023**, Kamati Ndogo ya PRC itahudhuria mkutano wa *Global Compact* kuhusu Wakimbizi (GCR) ambao kwa kiasi kikubwa unaendana na maono ya Kamisheni ya Umoja wa Afrika ya kusimamia hali za kiutu.

i) Mikutano ya Wakala na ya Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Wakimbizi iliofanyika mwaka 2023 ni kama ifuatavyo:

10 Machi 2023	-	Kikao cha Wakala wa kujiandaa na Majadiliano
28 Machi 2023	-	Majadiliano yalioyolenga: -
	-	Makabidhiano ya Wajumbe waliopita
	-	Kupitisha Mpango Kazi wa 2023.
4 Mei 2023	-	Kikao cha Dharura cha Wakala kujadili mgogoro wa Sudani na athari zake kwa nchi jirani.
1 Sept 2023	-	Kikao cha Wakala Kujiandaa na Majadiliano
13 Sept 2023	-	Majadiliano kuhusu: -
	-	Taarifa kwa UNHCR kuhusu ahadi za GRF,
	-	Mapendekezo ya AU kuhusu ahadi za GRF,
	-	Taarifa kuhusu Uendeshaji wa AfHA
	-	Hali ya Majanga nchini Libya na Morocco.
1 Dis 2023	-	Kikao cha Wakala kujiandaa na Kikao cha Majadiliano
4 Dis 2023	-	Kikao cha Majadiliano kuhusu: -
	-	Kuangazia Taarifa kwa Mkutano wa Kilele wa Jan/Feb 2024

IV. MAPENDEKEZO

51. Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Wakimbizi, Wakimbizi Wanaorejea, na Watu Walioyakimbia Makazi;

j) Inatoa wito kwa Nchi Wanachama wa AU na jumuiya ya kimataifa kusaidia hatua za kiutu katika nchi za Afrikan zilizoathiriwa zaidi na changamoto za kiutu kwa muda mrefu kwa kuzingatia zaidi ukanda wa Pembe ya Afrika, Sahrawi, Maziwa Makuu na ukanda wa Sahel.

k) Inatoa shukrani kwa Nchi Wanachama ambao wametimiza ahadi zao na kutoa wito kwa nchi ambazo bado hazijafanya hivyo kufanya hivyo haraka

inavyowezekana. Hatua za ufuatiliaji zaidi zinahitajika kwa nchi ambazo zilitoa ahadi kwenye Mkutano wa Ahadi wa Malabo kutimiza ahadi zao na kusaidia mahitaji ya kiutu barani Afrika.

l) Inahimiza Kamisheni kuhakikisha kwamba Wakala wa Kiutu wa Afrika unaanza kufanya kazi mapema mwaka 2024 ili kupunguza hali mbaya ya kiutu kwa watu walio katika hali hatari katika nchi mbalimbali zilizotembelewa wakati wa ujumbe wa tathmini.

m) Inaidhinisha pendekezo la ahadi lililotolewa na Kamisheni kuwasilishwa kwa Jukwaa la Wakimbizi Duniani likilenga utekelezaji wa Mshikamano wa Dunia kuhusu Wakimbizi.

n) Inaendelea kusisitiza haja ya kumaliza changamoto ya kiutu nchini Sudani na watu kukimbilia nchi za jirani (Chadi, Egypt, Ethiopia, na Sudani Kusini), ukanda wa Sahel, Ukanda wa Pembe ya Afrika na Ziwa Chadi, majanga yalioyoikumba Libya na Morocco na UKanda wa Kusini mwa Afrika.

o) Inatoa wito kwa Nchi Wanachama ambazo bado hazijatia sahihi au kuridhia Mkataba wa OAU wa mwaka 1969 na Mkataba wa Kampala wa mwaka 2009 kufanya hivyo, na zile ambazo zimesharidhia mikataba hiyo inahimizwa kuijumuisha kikamilifu kwenye sheria na sera zao za ndani ili kufanikisha utekelezaji fanisi katika ngazi za kitaifa na za chini.

p) Inazipongeza Nchi Wanachama kwa kutoa hifadhi kwa wakimbizi, watu wanaotafuta hifadhi na wahamiaji, na inatoa wito kwa mshikamano wa kimataifa na kusaidiana kubeba mzigo huo pamoja na nchi na jamii zinazotoa hifadhi.

V. HITIMISHO

52. Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Wakimbizi, Wakimbizi Wanaorejea na Watu Walioyakimbia Makazi yao inatoa shukrani kwa Serikali za Nchi Wanachama zilizotembelewa kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa ujumbe wa tathmini ya kiutu.

53. Kamati Ndogo ya PRC kuhusu Wakimbizi, Wakimbizi Wanaorejea na Watu Walioyakimbia Makazi pia inatoa shukrani kwa Mabalozi waliofanya tathmini kwa kipindi husika, na inahimiza Mabalozi wengine kujitoa kusaidia Kamati kufanya kazi hii adhimu.

AFRICAN UNION UNION AFRICAINE

African Union Common Repository **http://archives.au.int**

Organs Council of Ministers & Executive Council Collection

2024-01-15

Report of the 2023 activities of the PRC Sub-Committee on refugees, returnees, and internally displaced persons

African Union

African Union

https://archives.au.int/handle/123456789/10498

Downloaded from African Union Common Repository